# JE, MTU ALIYEOKOKA ANAWEZA KUCHAGUA KUPOTEA?

**JOE CREWS**

# JE, MTU ALIYEOKOKA ANAWEZA KUCHAGUA KUPOTEA?

Na Joe Crews

(Hotuba Na. 2 ya Mambo ya Kweli Yanayoshangaza)

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Can A Saved Man Choose To Be Lost - Kiswahili

# JE, MTU ALIYEOKOKA ANAWEZA KUCHAGUA KUPOTEA?

Uwezo wa kuchagua ni kipawa cha ajabu toka kwa Mungu. Hata hivyo, kuna uchaguzi mmoja ambao Mungu hakumruhusu kabisa mwanadamu kuutumia. Hakuna awezaye kuchagua kama atazaliwa akiwa mwenye dhambi au la. Uamuzi unaoyaathiri sana maisha yetu ulifanywa zamani, zamani sana na babu zetu. Hatuna uchaguzi wo wote kabisa kuhusu aina ya tabia tunayotaka kuwa nayo wakati ule tunapozaliwa. Tunazaliwa na asili ya dhambi. Isipobadilishwa itatupeleka kwenye mauti ya milele.

Lakini ingawa sisi tunazaliwa kama wenye dhambi waliopotea, Mungu anatupa uchaguzi wa kuibadilisha tabia ile. Ni uchaguzi wa mtu binafsi, uchaguzi bora ambao hakuna mtu awezaye kutunyang'anya. Bila shaka unahusika na uamuzi wa maana ambao mtu ye yote anakabiliana nao katika kipindi cote cha maisha yake. Uchaguzi huo unahusu kama mtu aendelee kubaki na tabia yake ya dhambi na kufa milele, ama apokee tabia mpya kwa njia ya imani katika Kristo na kuishi milele.

Kutofautiana kwingi kupo kuhusu aina ya uchaguzi uliotolewa kwa kila mmoja wetu. Mamilioni wanaamini kwamba Mungu anafungua mlango mara moja tu katika maisha ya mtu ili apate kufanya uamuzi wake, kisha anaufunga mlango huo milele. Ni kana kwamba Mungu anasema hivi, "Nitakupa wewe uamuzi mmoja tu ili upate kugeuka toka katika hali yako itakayokuletea maangamizi. Mara tu unapoamua kuokolewa, basi, huwezi kabisa kuchagua kupotea tena. Unapompokea Kristo ni uchaguzi wako wa mwisho utakaopata kuufanya kwa ajili ya maisha yako ya milele. Ukibadili mawazo yako baadaye na kukataa kutimiza wajibu wako unaoambatana na uamuzi wako huo, basi, utakuwa umechelewa mno kufanya hivyo. Haidhuru wewe uwe unatamani kwa kina na uaminifu jinsi gani ili upate kupotea na kutubia toba yako uliyoifanya, huwezi kuukwepa uzima wa milele. Hakuna kiwango cho chote cha uasi wako mkali, kufuru yako ya makusudi, au maisha yako ya dhambi unayoishi yatakayoweza kubadili uamuzi wako ule uliofanya kwa mara moja ulipotaka kuokolewa. Sitakuruhusu ufanye uchaguzi mwingine zaidi baada ya wewe kumpokea Yesu kama Mwokozi wako."

Kimsingi, hiyo ndiyo imani ya sehemu kubwa ya Wakristo wanaotetea fundisho lisemalo kwamba *muumini anayo dhamana ya uzima wa milele*. Kundi jingine la Wakristo lenye unyofu wa moyo kama huo linaamini kwamba *Mungu anauacha wazi mlango kwa ajili yetu ili sisi tuweze kubadili mawazo yetu wakati wo wote tunapotaka.* Wanaamini kwamba wokovu hautegemei tendo moja tu lisilobadilika au uchaguzi uliofanywa zamani, bali unategemea *uhusiano binafsi wa muumini na Kristo.* Uamuzi wa kuvunja uhusiano huo wa upendo unapofanyika kwa njia ya kufanya uasi wa makusudi, basi, muumini huyo anakoma kuwa muumini wa kweli, naye anapoteza uhakika uwao wote wa wokovu wake.

### Mamilioni ya Watu Wako Hatarini

Utata usiokuwa wa kawaida kuhusu hoja hii unaleta shari. Ikiwa iko dhamana ya uzima ule wa baadaye ambayo haina masharti yo yote kwa waumini wote, basi, hilo bila shaka ni fundisho la ajabu sana ambalo lipo. Lakini ikiwa si la kweli, basi, kwa hakika hilo ni mojawapo ya uzushi wa hatari

mno ulimwenguni. Mamilioni wangeweza kuokolewa au kupotea kutokana na uamuzi wao wanaofanya juu ya suala hili.

Hebu, basi, nikupe mfano mmoja kuhusu fundisho hilo jinsi siku kwa siku linavyowavuta watu kuchagua maisha yao ya milele. Katika mojawapo ya mikutano yangu mikubwa ya mahubiri palikuwa na zaidi ya watu mia moja waliokuwa wanahudhuria ambao walikuwa wamebobea [wamezama] katika imani hiyo isemayo kwamba watu wamewekewa dhamana ya uzima wa milele. Walifurahi sana kuisikia ile kweli ikifunuliwa na Biblia. Sabato ya siku ya saba [Jumamosi] iliwasisimua mno kwa sababu huko nyuma walikuwa hawajapata kuielewa kabisa. Wote walisadiki kabisa kwamba Jumamosi ndiyo Sabato ya kweli ya Maandiko, na kwa hamu kubwa waliyakubali pia mafundisho makuu ya unabii. Lakini katika watu hao mia moja ni wachache mno waliofanya uamuzi wa aina yo yote ile ili kuitii kweli ile. Kwa kweli wote walikuwa na matatizo ya Sabato kuhusiana na kazi zao. Ingemaanisha kwamba ingewaletea usumbufu mwingi, matatizo kiuchumi, pamoja na uwezekano wa kupoteza kazi zao endapo wangeifuata kweli ile yote kabisa kabisa. Kila mmoja miongoni mwa wale walioukataa ujumbe ule alinipa maelezo yale yale - "Sisi *tumeokoka tayari*," wakasema, "*wala hatuwezi kupotea*. Kwa nini sisi tujitie katika hatari ya kupoteza kazi zetu kwa kuishika hiyo Sabato? Tusingeweza kuokolewa zaidi ya vile tulivyokwisha kuokolewa sasa kwa kuitunza hiyo Sabato, halafu sisi tunayo hakika kwamba hatuwezi kupotea kwa kuivunja hiyo Sabato."

Je, unaona jinsi sababu yao ilivyopatana na fundisho lao hilo? Kwao wokovu ulikuwa haujaunganishwa na utii, au na kuendelea kukua kiroho. Ulitegemea kabisa juu ya wakati ule uliopita walipokata shauri kumpokea Kristo. Haidhuru kama wao waliyatii au hawakuyatii mafunuo ya ile kweli yaliyokuja baadaye, mambo hayo hayakuwa na athari zo zote juu ya maisha yao ya mwisho ya milele. Wao wangeweza kuivunja amri ya nne, amri ya saba, au zote, na bado wakajisikia kuwa wamewekewa dhamana ya uzima wa milele katika ahadi waliyoidai wakati ule "walipookolewa." Kwa hakika, watu hao waliamini kwamba kule kutokutii kwao [uasi wao] kungeweza kuathiri furaha na amani ya uhusiano wao, lakini kwamba kusingeweza kamwe kuathiri uhakika wa wokovu wao wa mwisho.

Ni dhahiri kwamba fundisho hilo linahitaji kuchunguzwa kwa kina. Mambo mengi yanahusu umilele yanategemea jinsi tunavyolikubali au kulikataa. Tunahitaji kuyajibu maswali kama haya: Je, tunaweza kugeuza mawazo yetu kuhusu kuokolewa? Je, tunautupilia mbali uwezo wetu wa kuchagua wakati ule tunapoongoka? Je, wokovu wetu unategemea uamuzi wetu mkuu mmoja tuliofanya kwa dakika moja takatifu, au je, tunalazimika kuendelea kukua katika neema ya Kristo iokoayo baada ya kufanya uamuzi huo? Je, Mungu anaweza kuzichukua dhambi zetu zinazotunajisi na kuziingiza katika ufalme wake mtakatifu? Kwa bahati nzuri, Biblia ina mamia kwa mamia ya mafungu mazuri, yanayoeleweka wazi, kuweza kuyajibu maswali hayo. Sote kwa pamoja tutayaangalia hayo, na pia tutachunguza mafungu machache ambayo yamefafanuliwa ili kulitetea fundisho hilo lisemalo kwamba "*Ukiokolewa mara moja, basi, sikuzote wewe utakuwa umeokolewa*" (Once Saved, Always Saved).

## Mbinguni Hakuna Dhambi

Akizungumza habari za Yerusalemu Mpya, Yohana alisema, "Na ndani yake *HAKITAINGIA KAMWE CHO CHOTE KILICHO KINYONGE* [KINACHOLETA UNAJISI (dhambi) – KJV.]." Ufunuo 21:27. Yesu alisema, "Heri *WENYE MOYO* [MAWAZO] SAFI; maana watamwona Mungu." Mathayo 5:8. Paulo aliandika tena na tena habari za wenye dhambi kuzuiwa kuingia mbinguni. Dhambi ndicho kitu pekee kinachomnajisi mtu mbele za Mungu, wala hakuna ye yote anayetenda dhambi kwa makusudi atakayeingia katika ufalme wake. Paulo aliandika hivi, "Au hamjui ya kuwa *wadhalimu* hawataurithi ufalme wa Mungu? MSIDANGANYIKE, *waasherati* hawataurithi

ufalme wa Mungu, wala *waabudu sanamu*, wala *wazinzi* … wala *wevi*, wala *watamanio*, wala *walevi*….” 1 Wakorintho 6:9,10.

Hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo kuingia katika ufalme wa Mungu kumefungamana na uzoefu wa imani wa dakika chache - au hata wa muda mfupi - uliopita. Wokovu ni uhusiano hai unaoendelea kukua kwa kushirikiana pamoja na yule Anayetoa uzima wa milele. Unahitaji kuwapo kwa mawasiliano yanayoendelea ili kuweza kuupokea. Uzima ule ule wa Mungu unaweza kugawiwa kwa wanadamu, lakini HAUPATIKANI KAMWE BILA KUWA NA MUUNGANO HAI NA KRISTO! “Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.” 1 Yohana 5:12.

Kama vile nguvu ya uumbaji wa Mungu ilivyo ya muhimu kuwapo daima ili kuutegemeza ulimwengu na kuzishikilia pamoja chembe zake ndogo mno, ndivyo uweza wake wa uungu unavyohitajika daima ili kuuhifadhi uzima wa kiroho moyoni. Mtu anapochagua kwa makusudi kujitenga mbali na Mungu, mawasiliano hayo hukatika na maisha yake ya kiroho hukoma kutiririka. Wala Mungu hataingilia kati kwa nguvu mapenzi ya mtu awaye yote kwa kufanya uchaguzi kwa niaba yake. Kwa ushahidi unaoonyesha kwamba *Wakristo wanaweza kupoteza uhusiano wao na Yesu na kupotea*, hebu soma Yohana 15:1-6. Hapo Kristo anaeleza mojawapo ya siri za uzima wa milele. “Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi; akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi hamwezi kufanya neno lo lote. *Mtu asipokaa ndani yangu*, *hutupwa nje* kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.” Fungu la 5 na 6.

## Siri ya Uzima Unaoendelea
## Ni Kuendelea Kukaa Ndani Yake

Zingatia ya kwamba siri ya uzima unaoendelea ni kuendelea kukaa ndani yake. Mtu asiyekaa ndani ya Kristo hunyauka, hufa, na hatimaye atachomwa motoni. Hii huthibitisha kwamba uhusiano kati ya muumini na Kristo si kitu kinachosimama pale pale kamwe, ambacho hutegemea uzoefu wa maisha uliopita. *Ni ushirikiano wa sasa hivi* wa pande zote mbili unaohusu maisha ya pamoja yatokayo kwake yeye “aliye uhai wetu.” (Kol. 3:4). Tawi linapotenganishwa na mzabibu, ndipo chimbuko lake la uzima hutoweka, na kifo peke yake ndicho kinaweza kutokea. Maneno haya ya Yesu yako wazi mno kuweza kueleweka vibaya. Hata Wakristo wale wamwaminio na kumtegemea, ambao wameunganishwa na huo mzabibu hai [Kristo], wanaweza kuchagua kujitenga mbali na mzabibu huo. Wakifanya hivyo, basi, wanakufa, nao watatupwa motoni na kuteketezwa. Hakuna kitu cho chote kiwezacho kunyauka na kufa ambacho hapo kwanza hakikuwa hai.

Dhamana ya uzima wa milele ni kwa wale tu ambao imani yao imekazwa milele kwa Yesu, na ambao maisha yao yameunganishwa na yule “aliye uzima wetu.” Ni dhahiri basi, kwamba tunaweza kuchagua kupotea haidhuru tuwe tulikwisha kuokolewa kwa jinsi gani wakati ule wa zamani. Kila kitu hutegemea katika kudumisha uhusiano huo mtakatifu pamoja na huo Mzabibu wa Kweli [Kristo]. Yesu alifundisha kweli ile ile nzito kuhusu kupoteza uzima wa milele katika mfano ule wa magugu. Katika kueleza maana ya mbegu zile zilizoanguka kati ya miiba na penye mwamba, Yesu alisema, “Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja Ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije **wakaamini na kuokoka**. Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha, nao hawana mizizi, **huamini kitambo kidogo**, na wakati wa kujaribiwa *hujitenga*.” Luka 8:12,13.

Yapo mambo kadhaa ya kuyazingatia kuhusu mfano huo. Kwanza, ni kundi moja tu hatimaye litakalookolewa - ni wale *waliozaa matunda sana*. Makundi yale yaliyowakilishwa kuwa yako karibu na njia na penye mwamba *hawataokolewa*. Katika fungu la 12 wasikivu wale waliokuwa kando ya

njia hawakupata nafasi ya "kuamini na kuokoka," lakini katika fungu linalofuata wasikivu wale penye mwamba wana"amini kitambo kidogo." Ni "kuamini" kwa jinsi gani huko? Kulingana na fungu la 12 huko ni kuamini kunakookoa. Kwa hiyo wale walioamini kitambo kidogo waliokoka kwa kitambo kidogo, lakini wakati wa kujaribiwa wakajitenga. Hatimaye, kusema kweli, walipotea pamoja na wale wengine wote, isipokuwa wale waliozaa matunda. Hapa lipo fundisho dhahiri la Bwana wetu lisemalo kwamba *watu wanaweza kuwa na imani ile iokoayo kwa kitambo kidogo, na, hata hivyo, wakaweza kuipoteza na wao wenyewe kupotea*.

## Dhamana ya Uzima ni ya Milele kwa Wale Tu Ambao Imani yao Imekazwa Milele kwa Yesu

Wale wanaosoma kwa makini kumbukumbu iliyoandikwa katika vitabu vya Injili watapata mamlaka ya Yesu inayolikanusha fundisho hilo la kuwekewa dhamana ya uzima wa milele. Katika Luka 12:42-46 Kristo alieleza katika mfano mwingine jinsi mtumishi mwaminifu alivyoweza kugeuka na kuwa mtumishi asiye mwaminifu. Baada ya kuuliza swali hili, "Ni nani, basi, aliye wakili mwaminifu, mwenye busara, ambaye bwana wake atamweka juu ya utumishi wake wote … ? Yesu analijibu swali lake mwenyewe, anasema, "Mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta anafanya hivyo … Atamweka juu ya vitu vyake vyote." Kisha Kristo anaeleza jinsi mtumwa yule ambavyo angeweza kupoteza fungu lake [thawabu yake]. "Lakini, mtumwa yule akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia kuja, akaanza kuwapiga wajoli wake, wanaume kwa wanawake, akila na kunywa na kulewa; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wasioamini."

Hapa upo mfano mkamilifu uliotolewa na Mwalimu Mkuu kuonyesha jinsi mtumwa yule mwaminifu, mwenye busara anavyoweza kuadhibiwa pamoja na wasioamini. Yesu alikuwa akiongea juu ya mtu aliyekuwa amemwona akiwa mwaminifu kiasi cha kutosha kumkabidhi madaraka makubwa. Bila shaka, mtumwa huyo huwawakilisha wale waliokuwa wamemtumikia Bwana kwa makini kama waumini wa kweli. Lakini kitu gani kilitokea kwake? *Mtumwa yule yule aliyekuwa mwaminifu aliiacha njia ile ya uaminifu na kuvuna maangamizi ya milele na mauti.* Je, jambo hilo halitukumbushi sisi pia maneno ya Waebrania 10:38, yasemayo, "Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye **akisita-sita**, roho yangu haina furaha naye." Mtumwa yule katika mfano huo, ambaye **alikuwa** muumini, sasa anaadhibiwa **pamoja** na wasioamini. Wale walio waaminifu wanaweza kurudi nyuma na kupotea.

## Wokovu Unaweza Kupotezwa

Mfano mmoja zaidi wa Kristo unaoonyesha wazi ukweli usemao kwamba kuendelea kupata msamaha hutolewa kwa muumini kwa sharti. Kisa hicho kinapatikana katika Mathayo 18:21-35, nacho kinahusu msamaha wa Mungu. Mfalme alikubali maombi ya mtumwa wake na kumsamehe deni lile kubwa. Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake aliyemdai kiasi kidogo tu, naye hakuonyesha huruma, akamtupa gerezani kwa sababu hakuweza kulipa. Mfalme yule aliposikia kile kilichokuwa kimetokea, *alibatilisha kitendo chake cha kulifuta deni lile kubwa na kumtupa mtumwa wake kwa watesaji hata atakapolipa deni ile yote.*

Hakuna mtu ye yote awezaye kukana mafundisho yaliyo wazi katika mfano huo. Ingawa Mungu anawasamehe kabisa wale wanaouomba msamaha huo, hiyo haimaanishi kwamba msamaha huo hauna masharti yo yote kwa maisha yale ya baadaye. Twaweza kuupoteza msamaha huo kwa kutokuwa na huruma kwa wengine. Hilo linaafikiana kabisa na maneno yake Bwana katika Ezekieli 33:13,

yasemayo, "Nimwambiapo mwenye haki, ya kwamba hakika ataishi, kama akiitumainia haki yake, *akatenda maovu*, basi katika matendo yake ya haki, hata mojawapo halitakumbukwa; bali katika uovu wake alioutenda, atakufa katika uovu huo." Kanuni hiyo imerudiwa tena katika fungu la 18, "Mwenye haki ageukapo, na kuiacha haki yake, **na kutenda maovu**, atakufa katika maovu hayo."

Siri yenyewe imo katika kudumisha uhusiano wa hiyo haki kwa kushirikiana pamoja na lile chimbuko la wokovu. Yesu alisema, "Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, **ndiye atakayeokoka**." Mathayo 24:13. Hakuna mtu ye yote atakayeokoka mwishoni ambaye hana tabia ya kupinga dhambi ya makusudi kwa uweza wa Mungu. Wale wasiovumilia hata mwisho [wanaokata tamaa njiani] majina yao yatafutwa katika kitabu cha uzima [Kut. 32:31-33; Ufu. 20:15]. Watetezi wa fundisho hilo lisemalo kwamba watu wanawekewa dhamana ya uzima wa milele, hukana na kusema kwamba jambo hilo haliwezi kutokea kamwe, lakini hebu soma wewe mwenyewe ujionee uwezekano uliopo unaotisha wa kutokea jambo hilo katika Ufunuo 3:5, "Yeye **ashindaye** … sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima." Maana yake iliyo wazi inaonyesha kwamba wale **wasioshinda** - yaani, wale **wasiovumilia hata mwisho** - majina yao **yatafutwa**.

Kwa kweli mafungu hayo yote yanasema kitu kile kile kimoja. Dhambi ya makusudi inauvunjilia mbali uhusiano huo ambao kwa huo uzima wa milele unapatikana. Kuna sharti la milele la "ikiwa" [yaani, kama, au –ki-, au –si-] katika kila wazo linalohusiana na dhamana ya uzima wa milele. "IKIWA [KAMA] hilo mlilolisikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu, ninyi nanyi mtakaa ndani ya Mwana, na ndani ya Baba." 1 Yohana 2:24. "Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani, naye aKIsita-sita, roho yangu haina furaha naye." Waebrania 10:38. "Mtu aSIpokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi. Yohana 15:6. "Mtu aKIlishika neno langu, hataona mauti milele." Yohana 8:51. "UKIkaa katika wema huo; KAMA sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali." Warumi 11:22. MKItenda hayo hamtajikwaa kamwe." 2 Petro 1:10. "Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, KAMA tuKIshikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho." Waebrania 3:14. "KAMA tuKIstahimili, tutamiliki pamoja naye; KAMA tuKImkana yeye, yeye naye atatukana sisi." 2 Timotheo 2:12. "KAMA tuKI fanya dhambi kusudi … haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Waebrania 10:26. "Mtu aKIipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." 1 Yohana 2:15. "Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mKItenda niwaamuruyo." Yohana 15:14. "KAMA mKIishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa." Warumi 8:13.

## Hatari ya Kukataliwa

Paulo alitambua kuwapo kwa uwezekano wa kutisha wa kukataliwa mbele za Mungu mwishoni, isipokuwa kama angeuzuia mwelekeo wa mwili wake unaompeleka kwenye dhambi. Yeye alisema hivi, "… Isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa." 1 Wakorintho 9:27. Neno hili - kukataliwa (reprobate) - analolitumia Paulo ni la kuvutia sana. Linatokana na neno la Kigiriki "adokimos," ambalo limetafsiriwa "mfisadi" mahali pengine. Kwa kweli, 2 Wakorintho 13:5 hutangaza kwamba Yesu Kristo hawezi kukaa katika moyo wa mtu aliyekataliwa (mfisadi) (adokimos). Tito 1:16 husema juu ya wenye machukizo na waasi ambao "kwa kila tendo jema hawafai (adokimos)." Ni hakika kwamba Paulo hakuwa na wazo jingine lo lote, ila lile tu la kwamba angeweza kupotea kama angeiruhusu dhambi kuyateka tena maisha yake.

Paulo pia anasema juu ya uwezekano wa waumini waliozaliwa mara ya pili wa kukabiliwa na hukumu kwa sababu wanapokea Meza ya Bwana isivyostahili. "Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili." Hakuna awezaye kukana kwamba watu hao walikuwa ni Wakristo waliojitoa hasa, walioshiriki katika ishara [mifano] zile za ukombozi wao. Je! hao wangeweza kuhukumiwa na kupotea? Paulo alisema kwamba wangeweza. Hukumu ni

nini? Neno lile lile la Kigiriki (krima) hupatikana katika 1 Timotheo 5:12. "Nao wana hukumu (krima) kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza." Ni dhahiri jinsi gani kwamba waumini wanaweza ku"iacha imani yao ya kwanza" na hatimaye kuingia katika hukumu.

Nimesikiliza mara nyingi sana maelezo yanayotolewa juu ya kuwekewa dhamana ya uzima wa milele ambayo yamejengwa juu ya mfano wa uana (sonship). "Mwanangu amezaliwa katika familia yangu, naye ataendelea daima kuwa mwanangu. Hawezi kuchagua kutokuzaliwa. Awe mtiifu au si mtiifu, daima atakuwa mwanangu." Mawazo kama hayo huikwepa hoja yenyewe. Hoja si kwamba mtoto huyo anaweza kuchagua "kutokuzaliwa," bali kwamba anaweza kuugua na kufa. Hakuna daktari ye yote anayewaonya wazazi wapya dhidi ya hatari zinazomkabili mtoto wao kwa kuchagua "kutokuzaliwa," bali ana mengi ya kusema juu ya matunzo yake mazuri ili kumzuia asife. Kwa kweli, mtoto huyo kama halishwi, atakufa upesi. Vile vile, Yesu alisema, "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu [Kristo] na kuinywa damu yake, **hamna uzima ndani yenu**." Yohana 6:53. Je, hivi alikuwa akiongea juu ya kitu gani? Katika fungu lile la 63 alifafanua, akasema, "Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena **ni uzima**." Mkristo asipoishi kwa Neno la Mungu, hawezi kuendelea kushiriki uzima wa kiroho utokao kwake.

Hivi tumethibitisha waziwazi kwamba *utii unaoendelea ni wa lazima kwa wokovu wetu wa mwisho*? Paulo aliandika hivi, "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii?" Warumi 6:16. Mtu anapochagua kuacha kumtii Kristo, halafu anamtii yule mwovu [Shetani] badala yake, basi, yeye si wake Kristo tena, bali ni wa Shetani. "Atendaye haki yuna haki … atendaye dhambi ni wa Ibilisi." 1 Yohana 3:7,8.

Mwandishi wa kitabu wa Waebrania anatoa maonyo maalum mengi dhidi ya kukengeuka kutoka katika imani. Waebrania 10:23 hufungua njia ya hoja ambayo hakuna mtu awezaye kuikanusha dhidi ya msimamo usemao kwamba ukiokolewa mara moja, basi, sikuzote wewe utakuwa umeokolewa. Kifungu cha maneno huanza kwa namna hii: "Na tulishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke." Kisha baada ya hayo, onyo linatolewa kwa wale ambao wangeweza kujaribiwa kuacha kukusanyika pamoja na waumini wenzao. Ni dhahiri kwamba hiyo ni mojawapo ya dalili za kurudi nyuma. Mwandishi wa waraka huo, mimi nadhani alikuwa Paulo, anajihesabu na yeye mwenyewe katika onyo hilo. Anaandika hivi, "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano **aliyotakaswa kwayo** kuwa ni kitu cha ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?" Maneno hayo ni kutoka fungu la 26 hadi la 29. Watu walioelezwa hapo walikuwa wametakaswa kwa ile kweli, lakini waliangukia katika uasi wa makusudi.

Basi, mafungu hayo ya mwisho ya sura hiyo hutoa onyo dhidi ya kuutupa ujasiri wao. Zingatia hilo kwa makini! "Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi … Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu." Mafungu kuanzia la 35 hadi la 39. Basi, mtu awaye yote angewezaje kusema kwa wazi zaidi ukweli ule usemao kwamba wokovu wa milele wa mwanadamu unapatikana kwa sharti la kuendelea kwake kuwa thabiti mpaka mwisho? Ila kama palikuwapo na uwezekano kwamba mmoja angeweza kuutupa ujasiri wake, yaani, kwamba angeweza kurudi nyuma na kupotea, kwa nini, basi, mtu huyo wa Mungu angelitoa onyo hilo kama vile alivyofanya?

Katika Waebrania 6:4-6 tunaupata usemi mwingine wa kushangaza sana. "Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, **wakaanguka** baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri." Basi, mimi nadhani ingekuwa vigumu sana kumweleza kwa kukamilifu zaidi ya huo mtu yule aliyekuwa amezaliwa mara ya pili, lakini ambaye baadaye alimwasi Mungu na kumkana Kristo na kumdharau Roho Mtakatifu. Amejiweka mbali kwa matendo yake mwenyewe mahali asipoweza kufikiwa na Mungu. Kwa hiyo, hakuna uwezekano wo wote kwa mtu kama huyo kuweza kuokolewa kadiri anavyoendelea kumsulibisha Kristo kwa kutotii kwake.

## Matawi Yaweza Kukatwa

Katika sura ya 11 ya Warumi, Paulo anaongea juu ya ukweli usemao kwamba wengi miongoni mwa wale waliozaliwa kimwili katika Israeli walimkataa Mwana wa Mungu na hivyo wakakatwa. Kielelezo kilichotumika ni mzeituni. Matawi yale walikuwa ni wana wa Israeli, lakini kutokana na kutokuamini kwao walikatwa, kama utakavyosoma katika fungu la 17 mpaka lile la 20. Ndipo matawi mengine ya mzeituni mwitu yakapandikizwa, ambayo yanawawakilisha Wakristo wa Mataifa. Basi zingatia onyo hili: "Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaachia matawi ya asili, wala hatakuachia wewe. Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, **ukikaa katika wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali**." Fungu la 21 na 22. Tafadhali zingatia kwamba dhamana iwayo yote ya uzima wa milele kwa matawi yale ilitegemea kabisa juu ya kuunganishwa kwao na mti ule. Dhamana yao ya uzima wa milele ilitolewa kwa masharti.

Hebu, basi, na tuone kama Petro anakubaliana na mawazo hayo ya Paulo. Katika waraka wake wa pili, sura ya kwanza, zimeorodheshwa tabia njema ambazo zingepaswa kuonekana katika maisha ya kila Mkristo. Hizo zimetajwa katika mafungu kuanzia lile la 5 hadi la 7, tena angalia kwamba anawaandikia "wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika haki ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo. Fungu la 1. Kisha walikuwa wamepewa "vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe." Fungu la 3. Ni dhahiri sana kwamba Petro anasema maneno hayo kwa wale waliokwisha kuongolewa. Lakini zingatia onyo analotoa: "Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana *mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe*." Fungu la 9 na 10. Hakika hayo huonyesha kwamba Wakristo wanaweza kuanguka kutoka katika neema. Wanaweza kurudi nyuma na kuacha kumfuata Yesu. Hata wanaweza kuwa waasi kwa maana halisi ya neno hilo. Kisha katika sura ile ya tatu Petro anaendelea kusema, "Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake." Fungu la 14. "Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu, mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu." Fungu la 17. Basi, twaona kwamba Petro anakubaliana na Paulo kwamba Wakristo wanahitaji kujilinda kila wakati wasije wakapotoshwa, tena anaonyesha hali ya mwisho ya kusikitisha ya wale wanaorudi nyuma na kuingia katika dhambi baada ya kuongoka kwao.

Kimojawapo cha vifungu vyenye nguvu kabisa katika Biblia kinachothibitisha kwamba mtu anaweza kugeuka na kwenda mbali na Kristo na kupotea hata baada ya yeye kukiri kwamba ameokoka, ni kile kilicho katika 2 Petro 2:20-22. "Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu

ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni." Fundisho lililopo hapo ni dhahiri.

Kwa hiyo, wale wanaochukua msimamo wao kutetea fundisho la "kupewa dhamana ya uzima wa milele bila masharti yo yote" wanasema kwamba wana wa Mungu hawawezi kuwakilishwa na mbwa na nguruwe. Vema, huenda hawawezi, lakini Petro aliwawakilisha hivyo - na ni kielelezo kizuri kabisa. Mithali hiyo iko wazi kabisa kwa namna ambayo inawaumiza wale wanaoikataa. Walikuwa wameyakimbia machafu ya dunia hii kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo. Walikuwa wameongoka. Walikuwa wamejiunga na Kristo na kusimama upande wake. Walikuwa wamempa maisha yao yote, lakini wakaikumbuka dunia na "kugaa-gaa" katika dhambi. Wanafanana naWaisraeli wale waliotoka Misri na kuyakumbuka yale "masufuria ya nyama," "mboga na vitunguu." Walizikumbuka anasa za dhambi; kwa hiyo wakamwacha Kristo na kurudi katika ulimwengu kama nguruwe anavyorudia kugaa-gaa katika matope yake. Kwa kweli Mkristo ye yote asiige tabia ya nguruwe, lakini mithali ya Petro inaonyesha kwamba jambo hilo linawezekana.

Roho wa Mungu hajanyamaza kimya kuhusu jambo hilo. Hebu sikiliza, asemavyo: "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho **wengi watajitenga na imani**, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Hilo litatokea lini? Ni lini ambapo wengine "watajitenga na imani"? Ni katika "nyakati za mwisho." Nyakati hizo zingekuwa ni wakati huu wa sasa, au sivyo? Hizo zingekuwa ni nyakati zetu hizi tunazoishi sasa pamoja na nyakati zilizo mbele yetu ambazo ziko karibu sana nasi. Kama hujapata kulifikiria hilo siku za nyuma, basi, hizi ndizo nyakati za hatari. Na kama wewe bado hujasadiki, basi, soma vichwa vikuu katika gazeti lo lote la kesho na kutafakari habari zake kwa makini.

Juu ya jambo hilo Roho anena "waziwazi." Neno hilo lina maana gani basi? Lina maana kwamba Roho anasema kwa maneno yanayoeleweka wazi, yaani, yaliyo dhahiri - yaliyo wazi mno kiasi kwamba haiwezekani kukosea kuyaelewa. Haya, basi, wengine wangefanya nini? Wengine wangejitenga na imani. Kwa hiyo, uwezekano upo wa kuiacha imani, au sivyo? Wengine hufanya hivyo. Wamekuwa katika imani, wameabudu pamoja na ndugu zao, wamekwenda kanisani na kuhudhuria mikutano ya maombi. Wamekuwa na bidii katika kuieneza injili, wametoa mali zao, wamekuwa wachungaji, maofisa wa kanisa, na walei mashuhuri; hata hivyo, wao wanaiacha imani. Hawajawa thabiti, wala waaminifu. Katika siku za mwisho zitakuja nyakati za hatari, pamoja na mateso na matatizo makubwa, na wengine hawawezi kusimama kidete. Wanajaribiwa na mambo ya dunia hii, na kudanganywa na roho za mashetani [mapepo]. Inasikitisha kusema hivi, kwamba wanautupilia mbali utii wao kwa yule Mtu wa msalaba. Walikuwa upande wake Kristo, lakini sasa wanasimama pamoja na adui yake.

Lakini hebu sikiliza - ukitaka "kuwekewa dhamana ya uzima wa milele isiyokuwa na masharti yo yote," unaweza kuipata. Imo ndani ya Kristo, kwa msingi wa kuwa na uhusiano naye wa **siku-kwa-siku**, na **dakika-kwa-dakika**. Unapompokea Kristo na kukaa karibu naye, utaweza kuvumilia. **Hakuna, wala hapawezi kuwapo na kushindwa ukiwa upande wake Kristo**. Yeye hashindwi - yeye ni mwaminifu. "Umtwike BWANA mzigo wako naye atakutegemeza." Zaburi 55:22. Atasimama kando yako kwa kadiri utakavyoendelea kusimama kando yake. Yesu alisema juu yake mwenyewe, "Mimi ndimi **Njia**, na **Kweli**, na **Uzima**." Yohana 14:6. Naye Yohana aliandika hivi juu ya Bwana, "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa **uzima wa milele**; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:11,12.

Wengi wasiokuwa Wakristo wanadhani kwamba wamepewa dhamana ya uzima wa milele. Wao watakuambia wanaamini kwamba Mungu atawaingiza mbinguni. Watasema, "Mimi ni mwema sawasawa na watu wale waliomo kanisani," au "Najisikia nitaokolewa pasipo kwenda kanisani." Lakini ukweli ni huu, hakuna mtu awaye yote anayeokolewa kwa kutegemea hisia zake. Anaweza kuwa mnyofu katika hisia zake, lakini unyofu wake huo hautamwokoa. Anaweza kuwa mwaminifu, mkweli, mwenye maadili mema, na raia wa daraja la kwanza, lakini hayo hayawezi kumwokoa. Anaweza kuwa mkarimu, mtu anayelisaidia kanisa lake kwa hali na mali na kuwapa maskini misaada mbalimbali, lakini hakuna mojawapo la hayo linaloweza kumwokoa. Hakuna mtu ye yote anayeokolewa kwa matendo yake, haidhuru yawe mema jinsi gani.

Kumbuka hili, na kulitafakari, usilisahau kamwe: Kristo ndiye Mwokozi, sio zawadi zako unazotoa, sio matendo yako mema unayotenda. Yeye anakupa wewe wokovu wake bure. Wokovu huo umo ndani yake Kristo, nawe unapompokea Kristo, basi, unakuwa na wokovu huo. "Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:12. Lakini ikiwa hunaye Mwana, basi, wewe huna huo uzima, wala huwezi kupewa dhamana ya uzima wa milele mpaka uwe naye na kuendelea kuwa naye Kristo, Mwana wake.

## Humaanisha Nini kwa Mkristo Kuuacha "Upendo Wake wa Kwanza"?

"Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha UPENDO WAKO WA KWANZA. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu." Ufunuo 2:4,5.

Kwa Mkristo kuuacha "upendo wake wa kwanza," ni **kurudi nyuma** [kuasi], **kuanguka** [dhambini], **kumwacha Bwana na kazi yake**, na **kwenda katika utumwa wa dhambi** kwa Shetani na ulimwengu huu. Mungu anawataka hao wote kutubu na kuyafanya "matendo ya kwanza" (kuzaa matunda ya upendo), la sivyo, - la sivyo nini? "Nitakiondoa kinara chako katika mahali pake." Hilo ndilo neno la mwisho toka kwa Bwana. Mwenye dhambi akikubali, akitubu, akirudia upendo wake wa kwanza, na kufanya matendo yake ya kwanza, basi, mambo yote kwake huwa mema - huyo ataokolewa. Lakini uchaguzi ni wake. Asipofanya hivyo, basi, nuru yake huondolewa, yaani, huzimika, na mtu yule aliyerudi nyuma kwa njia hiyo anapotea.

## Je, Ni Jambo la Kawaida kwa Yule Aliyerudi Nyuma Kumrudia Bwana Kabla ya Siku Yake ya Kufa?

La, ni mbali na hilo. Hayo ndiyo yaliyompata mfalme wa kwanza wa Israeli, Sauli. Imeandikwa kumhusu Sauli kwamba a"tageuzwa na kuwa mtu mwingine." "Na Roho ya BWANA itakujilia kwa nguvu, nawe utatabiri pamoja nao, nawe UTAGEUZWA KUWA MTU MWINGINE." 1 Samweli 10:6. Lakini Sauli alirudi nyuma kutoka katika cheo chake cha juu kilichotukuzwa, **hakumtii Bwana**, na mwishowe alijiua (1 Samweli 31:1-6). Katika jambo hilo haiwezi kusemwa kwamba Sauli alikuwa hajaongoka, kwa sababu Mungu anasema kwamba aliongoka - lakini, alijiua mwenyewe, wala hakupata na nafasi yo yote ya kutubu.

## Hakuna Mtu Awezaye Kuwapokonya

Mwisho, hebu na tuliangalie fungu la maneno ambalo huenda limenukuliwa sana kuliko jingine liwalo lote ili kuliunga mkono fundisho lisemalo kwamba watu wanawekewa dhamana ya uzima wa

milele. Yesu alisema, “Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.” Yohana 10:28,29.

Hiyo ingekuwa ni ahadi kuu ilioje kwa kila mwana wa Mungu anayemtegemea! Ukiangalia kwa haraka-haraka kwa mara yako ya kwanza linaonekana kana kwamba ni dhamana ya aina fulani ya kupewa kinga dhidi ya hasara ya kiroho, lakini basi, bado hatujalisoma fungu lote. Fungu la 27 ni sehemu kamili ya wazo hilo, nalo linaweeka masharti maalum ili ahadi hiyo iliyo katika fungu la 28 na 29 ipate kutimizwa. “Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata.” Tafadhali zingatia ya kwamba ni wafuasi wale wa kweli tu wa Mungu wanaokaa salama katika mkono wake unaowalinda. Anawapa uzima wa milele kondoo wale tu walio waaminifu, wanaomsikia na kumfuata. Ni usikuvu wao huo na huko kumfuata kwao ambako huwapatia kinga dhidi ya kupokonywa na ibilisi au na vibaraka wake. Ulinzi huo ni dhidi ya maadui walioko huko nje ambao wanajaribu kuwachukua kondoo na kwena nao mbali, lakini ulinzi huo si kwa kondoo wale waliokosa uaminifu ambao wangeweza kuchagua kutokuendelea tena kumfuata. Hakuna mtu ye yote awezaye kuwapokonya hao katika mkono wa Baba yake, lakini basi, wao wanaweza kuchagua kuruka na kwenda nje wakati wo wote ule wanapopenda. Mungu hadokezei hapo kabisa kwamba ataingilia kati na kuwanyima wafuasi wake uhuru wao wa kuchagua. **Wakristo wanaweza kuchagua kupotea kwa hakika sawasawa na vile wenye dhambi wanavyoweza kuchagua kuokolewa**.

Hebu fikiria jinsi ambavyo yasingekuwa na maana mamia kwa mamia ya maonyo ya Biblia dhidi ya uasi kama uwezekano wa kuasi usingekuwako. Kwa nini Roho angekuwa amewaongoza akina Paulo, Petro, na wengine wote kuandika vitisho na maonyo hayo ya kutisha dhidi ya kupotea milele kama wasingekuwa katika hatari yo yote ya kupatwa na jambo hilo? Na kama ni kweli kwamba wale waliookolewa-mara-moja wamepewa dhamana ya uzima wa milele, basi, ni hakika Ibilisi angejua. Basi, asingepoteza kamwe wakati wake wo wote juu ya waumini, akijua jinsi isivyowezekana kabisa kwake kuwafanya wapotee. Hata hivyo, sisi sote tunajua kwa uzoefu wa maisha yetu ya kwamba Shetani anafanya kazi yake kwa juhudi nyingi zaidi ili kuwavuta na kwenda nao mbali watakatifu wasipate kumfuata Kristo.

Yatupasa kuhitimisha kwa kusema kwamba wokovu hautegemei kujitoa mara moja tu, ambako hakuwezi kutanguka, kuwe ni kwa wakati uliopita au wakati wa sasa. Kuokolewa ni uzoefu wa kuishi maisha yanayofanana na yale ya Kristo ambayo kwanza tunapewa kwa uweza wa Mungu, halafu yanakuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Wokovu si kitu halisi tunachoweza kukishika kwa mkono, ila ni uhusiano ulio hai kati yetu na Kristo, Chimbuko la uzima wa milele, ambao unapaswa kuendelezwa daima. Kuokolewa ni lazima kuongelewe habari zake katika nyakati tatu za wakati [Wakati Uliopita, Wakati wa Sasa, Wakati Ujao] ili kuafikiana kabisa na Biblia. **Umetokea**, **Unaendelea Kutokea**, na **Utatokea**. Pengine mfano huu wa Glenn Fillman utasaidia kuelezea jambo hilo.

### Kuokolewa - Wakati Uliopita,<br>Wakati wa Sasa na Wakati Ujao

Bill Jones anavua samaki maili kadhaa ndani ya bahari. Mashua yake inapinduka na kuzama mpaka chini kilindini. Yeye hawezi kuogelea ili kwenda kwenye usalama. Wakati uo huo mashua nyingine ya uvuvi inakuja, lakini imejaza shehena nzito mno kiasi kwamba haiwezekani kumchukua abiria mwingine. Walakini, kwa kuwa wanataka kumwokoa mtu yule anayeangamia, mabaharia wale wanamtupia kamba. “Haya! Shika kamba hiyo,” wanamwambia. “Tutakuvuta hadi ufukoni [pwani].” Anapoishika kamba ile Bill Jones anasema, “Asante Mungu, **Nimeokoka**!” Naye **anaendelea**

**kuokolewa kwa muda wote anaoendelea kuishikilia kamba ile**. Wokovu ni wake, lakini anayo sehemu yake ya kufanya katika wokovu huo. Endapo kwa wakati wo wote ule angeiachilia kamba ile na kukataa kuishika tena, basi, angeangamia. Ndivyo ilivyo kwa mtu aliyeokolewa kutoka dhambini. Anaendelea kuokolewa kwa muda wote anaoendelea kuushika mkono wa Kristo. Kama angeamua kuuachilia mkono ule na kuushika mkono wa Ibilisi, basi, angeweza kupotea. Wokovu wake unategemea uamuzi wake na hatua ile anayoichukua katika kuupata.

Kwa kweli, mtu anaweza kuongea kwa usahihi juu ya wokovu katika nyakati tatu - wakati uliopita, wakati wa sasa, na wakati ujao. Anaweza kusema, "Nimeokolewa" anapoishika ile kamba, "Ninaendelea kuokolewa" anapoendelea kuvutwa kuelekea ufukoni, na "Nitaokolewa" anapoikita kwa nguvu miguu yake ufukoni. Mtu aliyeongoka **ameokolewa** kutoka katika adhabu ya dhambi. Kitendo hicho tunakiita Kuhesabiwa Haki (Justification). **Kwa wakati huu wa sasa anaendelea kuokolewa** kutoka katika uwezo wa dhambi, na kitendo hicho tunakiita Utakaso (Sanctification). **Ataokolewa** kutoka katika kuwapo kwa dhambi wakati ule atakapokuja Kristo, na kitendo hicho kitakuwa ni Kutukuzwa (Glorification). Nyakati zote tatu hutumika katika Biblia kuhusiana na kuokolewa.

Katika Warumi 8:24 tunapata usemi usemao, "Tuliokolewa [twaokolewa – KJV] kwa taraja [tumaini]. Tafsiri ya Weymouth ni sahihi zaidi. Anasema, "<u>Tumeokolewa</u>," wakati uliopita. Tafsiri ya Toleo la Revised Standard hukiweka kwa usahihi kifungu kile cha maneno kilicho katika 1 Wakorintho 1:18 kama hivi, "Kwetu sisi <u>tunaookolewa</u>." Halafu katika Matendo 15:11 husema "kwamba <u>tutaokoka</u> kwa neema ya Bwana Yesu." Basi, unauona wakati uliopita, wakati wa sasa, na wakati ujao.

Hebu sasa na tuhakikishe kwamba hakuna mtu anayepata picha mbaya kutokana na kielelezo chetu cha mtu yule anayeokolewa asizame majini. Je, ukweli kwamba anapaswa kuishikilia sana ile kamba ili kuokolewa una maana kwamba tunaweza kufanya kazi ili kupata huo wokovu kwa matendo yetu wenyewe? Hivyo sivyo kabisa, La! mara elfu. Kumbuka ya kwamba alikuwa akivutwa kwa nguvu nyingine kuliko ile yake. Alikuwa anashirikiana tu na uwezo ule. Alikuwa anaendelea kuishikilia ile kamba. Ilimpasa kufanya vile ili kuweza kuvutwa mpaka mahali pa usalama. Sisi kama Wakristo yatupasa kukiri imani yetu katika Kristo, hatuna budi kuendelea kuwa thabiti kwake, tunapaswa kuzaa matunda ya utii; hiyo ndiyo sehemu yetu katika kuendelea kumshikilia Kristo. Yeye hatatuachilia kamwe kwenda zetu. Njia pekee inayoweza kutufanya sisi tujitenge mbali naye ni ile ya sisi wenyewe kukomesha uhusiano wetu naye kwa makusudi na kujitenga mbali naye, lakini uwezo wa kufanya hivyo tunao. Sisi bado ni wajumbe walio huru kimaadili [kitabia]. Nia yetu haijaondolewa ndani yetu kutokana na sababu ya kwamba sisi tu Wakristo.

Mahali po pote katika safari ya maisha yetu ya Kikristo tunaweza kuamua kurudi nyuma, yaani, tunaweza kuchagua mambo ya dunia hii kuliko mambo ya Mungu na yale ya mbinguni. Tunaokolewa kwa njia ya imani peke yake katika Yesu Kristo kama Mwokozi wetu. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12. Kwa hali yo yote ile, sisi tunaonyesha imani yetu kwa matendo yetu [Yak. 2:17-22,26]. Hayo yanadhihirisha upendo wetu kwake. Kuzishika amri [kumi] za Mungu na kutenda haki ni matokeo tu ya kazi ya Roho Mtakatifu anayekaa moyoni mwetu. Hayo [matendo] ndiyo matunda ya Roho. Tunafanya mambo hayo, si kwa sababu tunataka kuokolewa, bali kwa sababu tumeokolewa [Efe. 2:8-10], na kwa kadiri tunavyoendelea kumpenda Bwana kwa moyo wetu wote, ndivyo kadiri tutakavyoendelea kuwa watiifu kwake. Hatutaiachilia ile kamba. Tutaendelea kumshikilia sana Kristo kama tumaini letu la pekee.

---

**ANGALIA:** Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [ ] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza zaidi. Yasinukuliwe.